Uhuru Uk. Tarehe 07/10/2020

# Profesa Kabudi aahidi kutatua migogoro ya wakulima, wafugaji

**Na LATIFA GANZEL,** *Morogoro*

MGOMBEA Ubunge Jimbo la Kilosa Kati kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Profesa Paramagamba Kabudi, amewaahidi wananchi wa jimbo hilo kuwa, atahakikusha anashughulikia migogoro ya wakulima na wafugaji.

Pia, ametaja vipaumbele vyake vingine 11, ambavyo atavishughulikia katika kipindi cha miaka mitano, akiwa mbunge wa jimbo hilo huku akiwaomba wananchi wamuamini na wampe ushirikiano.

Profesa Kabudi, aliyasema hayo juzi, katika Kata ya Dumila, wakati wa uzinduzi wa kampeni za CCM, katika jimbo hilo huku akitaja vipaumbele hivyo kuwa ni kumaliza migogoro ya wakulima na wafugaji, inayotokana na ardhi na kufufua zao la mkonge, ambalo lilikuwa likilimwa tangu enzi ya utawala wa mkoloni

Alisema katika kumaliza migogoro ya wakulima na wafugaji, atahakikisha wilaya yote ya Kilosa, inafanyiwa mpango wa matumizi bora ya ardhi na kwamba, tayari Wizara ya Ardhi imeshaanza kutenga fedha kwa ajili ya mpango huo.

Profesa Kabudi, alisema yapo mashamba 49, ambayo Rais Magufuli, ameshayafutia hatimiliki zake na mengine yapo kwenye utaratibu wa kufutwa.

"Kanuni za uchaguzi zinanizuia kuyataja mashamba hayo, niwahikikishie wananchi wa Kilosa, mara baada ya zoezi la uchaguzi kumalizika, kazi ya kuwagawia wananchi ardhi ya mashamba hayo itaanza," alisema Profesa Kabudi.

Alisema kabla ya kugawa mashamba hayo, atahakikisha uhakiki wa kubainisha watu wenye mahitaji ya ardhi unafanyika, hiyo itasaidia kupunguza mwngiliano wa wakulima na wafugaji.

Akizungumzia kipaumbele cha kufufua zao la mkonge, Profesa Kabudi, alisema tangu enzi za utawala wa mkoloni, Wilaya ya Kilosa, ilikuwa ni ya kimkakati, ndio maana walianzisha mashamba makubwa ya mkonge, ambao ulikuwa ni moja ya mazao makubwa ya biashara.

Hivyo alisema katika kipindi cha uongozi wake, akiwa mbunge wa jimbo hilo, atahakikisha zao hilo ambalo kwa sasa lina thamani kubwa katika soko la dunia, linafufuliwa na linawanufaisha wananchi wa Kilosa.

Alitaja vipaumbele vingine, ambavyo vimekuwa changamoto kwa wananchi ni kuboresha miundombinu ya barabara, maji, umeme, kuongeza shule za msingi, sekondari, kuwezesha uanzishaji wa viwanda vidogo vya kusindika mboga na matunda, kuanzisha masoko ya nafaka.

Profesa Kabudi, alisema ana amini kuwa ahadi zote alizotoa, anaweza kuzitekeleza endapo wananchi wa Kilosa watamchagua Rais Dk. John Magufuli na madiwani wa CCM.

Alisema kitendo cha Rais Dk. Magufuli, kumpa ruhusa na kutambulishwa kwa wananchi wa Kilosa, ambao wamempitisha bila kupigwa, ni heshima kubwa kwake na chama chake, hivyo analo deni kubwa kwa wananchi hao la kuwatumikia na pia kwa Rais kuhakikisha anatekeleza na kuisimamia Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

Kwa upnade wake, Mwenyekiti wa CCM, Mkoa wa Morogoro, Innocent Kalogeres, alisemamkoa huo una majimbo 11, ambapo kati ya hayo, sita wagombea ubunge wa CCM wapitita bila ya kupingwa.

Kalogeres, alisema wilaya ya Kilosa ina jumla ya kata 25, ambapo kati ya hizo, 15 wagombea udiwani wa CCM wamepita bila ya kupingwa.

Hata hivyo, alisema kazi kubwa ipo kwa viongozi wa CCM, kuhakikisha kata 10, zinapata ushindi, likiwemo Jimbo la Mikumi, ambalo kwa miaka mitano iliyopita, lilikuwa likiongozwa na Joseph Haule, maarufu Profeasa J wa Chadema.

Scanned with CamScanner

Mtanzani uk. 8 ,
07/10/2020

# Watakiwa kuepuka madaktari bandia wa mifugo

Na RAYMOND MIHAYO

WAFUGAJI wa Mbwa na Paka Wilayani Kahama Mkoani Shinyanga wametakiwa kuacha kuwatumia Madaktari ambao hawana ujuzi kwa ajili ya matibabu ya mbwa wao hali ambayo inaweza kuleta madhara kwa wanyama hao katika siku za baadaye na pengine kusababisha vifo.

Kutokana na hali hiyo kuwepo mjini Kahama ni bora wakawatafute Madaktari au Maafisa wa Serikali ambao wanaojishughulisha na Kilimo na mifugo na kupata maelekezo ya wapi wanaweza kupata huduma hiyo kwa haraka.

Hayo yalisemwa juzi na Master Afshil Malik George, kiongozi kutoka katika Shirika la Kutetea Haki za Wanyama Tanzania (TAPO) wakati wa maadhimisho ya siku ya kichaa cha Mbwa ilifanyika mjini Kahama na kuendesha zoezi la channjo kwa mbwa.

George alisema kuwa katika Wilaya ya Kahama kuna baadhi ya madaktari ambao hawana ujuzi ambao wamevamia fani hiyo na kujihusisha na kutibu Wanyama aina ya mbwa nap aka hali ambayo inaweza kudhara wakati wowote.

Alisema kuwa shirika lake limekuwa likipata malalamiko mengi kutoka kwa Wananchi kuwa kuna baadhi ya watu wamemgia mitaani na kuendesha zoezi la chanjo mitaani na kupelekea mbwa wengi nap aka kufa.Alisema kuwa watu hao wamekuwa wakitumia maji kama dawa za minyoo na kuwachanja mbwa na paka na kupelekea Wanyama hao kufa mara nyingi kutokana na kupewa dawa hizo ambazo hazina kiwango kutoka kwa madaktari hao anbao hawana ujuzi.

"Kesi hizo zipo mara nyingi wanawang'ata watu ambao tayari wamekuwa wamechomwa chanjo ya kuzuia kichaa lakini wagonjwa wanapopimwa wanakutwa na tayari wamepata kichaa cha mbwa na kuwa na kesi nyingi zinazotokana na hali hiyo.

Aliendelea kusema kuwa kutokana na hali hiyo mwitikio wa wananchi kuchanja wanyama hao ni mkubwa ambao utanatokana nakesi hizo za mbwa na kuongeza kuwa wafugaji wamekuwa wakiwasumbua maofisa afya kwa ajili ya kuwapa chanjo Wanyama wao kwa wakati.

Kwa upande wake, mmoja wa wafungaji wa mbwa Mjini Kahama, Debora Moriss alisema kuwa amehamasika kufuga mnyama aina ya mbwa kutokana na kumsadia asingiliwe na vibaka na kuongeza kuwa mnyama huyo amekuwa ni mwepesi wa kutambua wahalifu kutokana na kuweza kunusa kwa kiwango kikubwa.

Scanned with CamScanner

Nipashe

# Sekta mifugo ichochee safari uchumi mkubwa

**WAKATI** Tanzania inaelekeza jitihada zake kufikia uchumi mkubwa kwa lugha nyingine, uchumi wa viwanda, mipango na mikakati sasa hainabudi kuangalia sekta ya mifugo kwa jicho la pili.

Hiyo ni kutokana na sekta ya mifugo kuwa na fursa nyingi za kuwezesha viwanda vyetu kuzalisha zaidi, kupitia kuvipatia malighafi zinazotokana na mazao yanayopatikana ikiwamo nyama, maziwa na ngozi.

Kwa sasa Tanzania inatajwa kuwa nchi ya pili kwa kuwa na idadi kubwa ya mifugo barani Afrika. Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Mifugo), Prof. Hezron Nongwa, kwa wahariri wa vyombo vya habari, Tanzania ina zaidi ya ng'ombe milioni 33, mbuzi milioni 22, kondoo milioni 5.6, punda zaidi ya 600,000, kuku milioni 83 na nguruwe 2,000,000.

Alieleza pia kwamba sekta ya mifugo kwa sasa inachangia asilimia 7.5 katika pato la taifa. Takwimu hizo na mchango wa sekta hiyo kwa pato la taifa ni ujumbe tosha kuhusiana na umuhimu wake katika safari ya kuelekea kwenye uchumi mkubwa wa viwanda baada ya nchi yetu kufanikiwa kuingia rasmi katika uchumi wa kati hivi karibuni.

Hatua kadhaa tunaona kuwa lazima zichukuliwe na serikali, wataalamu, wafugaji na wadau wengine kuboresha na kuipaisha sekta ya ufugaji ili iweze kuchangia inavyostahili katika safari ya uchumi wa viwanda. Kwa kiasi fulani kuna mafanikio yamepatikana kwa upande wa chanjo cha magonjwa mbalimbali ya mifugo, ingawa lengo la serikali ni kupata chanjo za magonjwa yote 13 ya mifugo. Magonjwa ya mifugo yanatajwa kuwa kikwazo kikubwa kwa maendeleo ya mifugo, ambapo Prof. Nongwa anasema magonjwa yanachangia vifo vya mifugo kwa asilimia 60.

Katika jitihada hizo, Taasisi ya Chanjo ya Kibaha mkoani Pwani, imeanza kuzalisha matokeo chanya baada ya kuonekana kufanikiwa kudhibiti kwa asilimia 95 ugonjwa wa mdondo unaowapata kuku wa kufuga.

Akizungumza na wahariri wa vyombo vya habari waliotembelea katika taasisi hiyo kushuhudia shughuli za utengenezaji wa chanjo za kudhibiti magonjwa ya mifugo zinazofanywa na taasisi hiyo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi Sekta ya Mifugo, Prof. Elisante Ole Gabriel, alisema mafanikio hayo ni kwa wafugaji waliozingatia kuchanja kuku wao mara tatu kwa mwaka kama inavyoelekezwa na wataalam wa mifugo.

Pia inaelezwa kuwa chanjo hiyo pia imesaidia kudhibiti ugonjwa wa ndorobo kutoka asilimia 32 hadi asilimia 60 katika maeneo mbalimbali nchini, yakiwamo ya hifadhi za taifa, kwa mujibu wa Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania, Dk. Furaha Mramba. Tunaipongeza serikali kwa kuamua kuweka msukumo kwa kuamua kuzalisha chanjo nchini kwa kuwa hatua hiyo itaepusha uwezekano wa hujuma za kiusalama ikiwa zitatoka nje pamoja na gharama kubwa za kuziagiza nje.

Ushauri wetu ni kuwa serikali iendelee kuiwezesha Mamlaka ya Maabara ya Veterinari Tanzania kibajeti ili itekeleze mkakati maalum wa kuzalisha chanjo za magonjwa yote 13.

Hatua nyingine muhimu ya kuhimiza na kuzingatiwa ni kwa wafugaji kujenga utamaduni wa kuwashirikisha na kuwatumia wataalamu wa mifugo kujua chanzo sahihi cha magonjwa yanayoikabili mifugo yao badala ya kujigeuza wao madaktari wa mifugo.

Hilo ni miongoni mwa mambo ambayo Prof. Gabriel, aliyahimiza, kwa kusema kuwa kuna baadhi ya wafugaji wanadhani kuwa ng'ombe ni wao, wanadhani wanaweza kuwa madaktari wakati sio kweli. Kwamba wafugaji lazima wawatumie wataalamu wa mifugo waambiwe chanzo sahihi kinachoikabili mifugo yao badala ya kukimbilia kuwapa chanjo au dawa wanazozijua we-





Na Sa
Kasik

Scanned with CamScanner

# *Govt in talks with NIC to have livestock insurance*

By Guardian Reporter

Permanent Secretary in the Ministry of Livestock and Fisheries, Prof Elisante ole Gabriel, has said that the ministry has initiated talks with the National Insurance Corporation (NIC) for the establishment of livestock insurance.

Prof Gabriel disclosed this at the weekend during his visit at Kibaha Tanzania Vaccine Institute under Tanzania Veterinary Laboratory Agency (TVLA).

He said they have already held talks with the NIC director general Dr Elirehema Doriye, adding that the talks were going on well.

Meanwhile, Prof Gabriel urged herders in the country to cooperate and make use with livestock experts to understand the real causes of diseases inflicting their livestock instead of doing the job themselves.

"There are some livestock keepers who think they own the cattle, and that they can become doctors, even if he owns a dispensary, he must involve a veterinary officer who must know how the animal is to be treated," said Prof. Gabriel. He added: "My call to livestock keepers is that they have to use veterinary experts who are to tell them the causes of the diseases afflicting their animals, they should abandon the belief that if they gave them a DTT injection, then all bacteria for anthrax will disappear, no."

He said livestock keepers must receive vaccinations at low cost and they should embrace modern practices in livestock keeping, and must ensure they buy the approved vaccination drugs.

He advised local councils to accord priority to the livestock sector in accordance with the law, and directed that 15 per cent of their internal revenues should be ploughed back to the development of the sector.

Prof Gabriel also called on livestock experts to offer their professional expertise to help herders.

Scanned with CamScanner